JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI



# SAFARI YA MIAKA NANE YA MHE. JUMAA AWESO (Mb) WIZARA YA MAJI

# YALIYOMO

Utangulizi

Uk. 4

Historia ya Uongozi katika Wizara ya Maji

(Mawaziri)

Uk. 10

Miaka Nane ya Mafanikio Makubwa Sekta ya Maji

Uk. 12

Mambo ya Kipekee Kuhusu Mhe. Waziri Jumaa

Aweso (Mb)

Uk. 27

Hitimisho

Uk. 35

# Kutoka Mwalimu wa Kemia Hadi Shujaa wa Sekta ya Maji: Safari ya Miaka Nane ya Jumaa Aweso Kubadili Taswira ya Sekta ya Maji Tanzania



Alipozaliwa tarehe 22 Machi 1985 katika Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga, tarehe ambayo pia huadhimishwa kote duniani kama Siku ya Maji - ilikuwa kana kwamba ni mpango wa Mungu, kwamba kijana huyu alizaliwa mahsusi kwa ajili ya kusimamia na kushughulikia Sekta ya Maji nchini Tanzania. Ni kama alikuja duniani kwa wakati maalum, ili atumike kama chombo cha kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi na salama. Kati ya mamilioni ya watu, si jambo la kawaida kuona mtu kuzaliwa siku yenye maana hiyo kubwa kimataifa, na baadaye kuwa kiungo muhimu katika kusimamia masuala hayo hayo ya maji kwa taifa zima.

Safari ya elimu ya Mheshimiwa Aweso ilianza katika Shule ya Msingi Mwambao, Pangani, kati ya mwaka 1994 hadi 2000 na baadaye aliendelea na Elimu ya Sekondari katika Shule ya Sekondari Bagamoyo kati ya mwaka 2001 hadi 2004. Alijiunga na Shule ya Sekondari Pugu kwa Elimu ya Juu ya Sekondari kuanzia mwaka 2005 hadi 2007. Kati ya mwaka 2007 na 2009, Aweso alipata Astashahada ya Ualimu kutoka Chuo cha Ualimu Morogoro, hatua iliyomjengea msingi wa kufundisha na kuwasiliana na jamii.

Pamoja na hayo, Aweso aliendelea na masomo ya juu na kupata Shahada ya Sayansi katika Kemia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2013. Baada ya kuingia katika siasa, alitambua umuhimu wa kuwa na maarifa ya utawala bora, hivyo kujiendeleza tena kwa Shahada ya Uzamili ya Utawala na Uongozi (Governance and Leadership) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kati ya mwaka 2018 hadi 2020.

Aweso alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Pangani mwaka 2015 kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), akiwakilisha wananchi kwa awamu yake ya kwanza. Ufanisi wake ulijitokeza mapema, na hivyo kupelekea kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji mwezi Oktoba 2017, nafasi ambayo ilimuweka karibu zaidi na changamoto halisi zinazowakabili Watanzania katika upatikanaji wa huduma ya maji.

Katika nafasi hiyo ya Naibu Waziri, Aweso alionesha uwezo mkubwa wa kuongoza kwa vitendo. Alikuwa akitembelea miradi ya maji nchi nzima, kusikiliza wananchi na kuhakikisha kuwa malalamiko yao yanapata ufumbuzi wa haraka. Sifa ya kutembelea maeneo ya vijijini na mijini bila kujali umbali wala hali ya miundombinu ilimfanya apendwe na wananchi wengi. Kwa wengi, Aweso si kiongozi wa ofisini bali mtu wa vitendo.

Kutokana na juhudi na bidii hizo, Oktoba 2020, Aweso alirudi bungeni baada ya kupita bila kupingwa, na mwezi Desemba 2020 aliteuliwa kuwa Waziri kamili wa Maji. Kuanzia hapo, alisimamia mageuzi makubwa katika sekta hiyo, akihakikisha kuwa sera, sheria na taratibu zinaboreshwa ili kuwasaidia wananchi kupata huduma ya majisafi na salama.

Chini ya uongozi wake, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) awamu ya pili ilitekelezwa kwa kasi mpya, na msingi wa awamu ya tatu (WSDP III) kuwekwa. Aweso alihakikisha kuwa mpango huo unazingatia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, usawa wa kijinsia, na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji. Kupitia jitihada hizi, Tanzania imepiga hatua kubwa katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG Goal 6).

Moja ya mafanikio makubwa ya Aweso ni kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Maji, ulioundwa chini ya Sheria Namba 5 ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019.

Kupitia Mfuko huo, miradi mingi ya maji vijijini na mijini imeweza kupata fedha kwa wakati, jambo ambalo hapo awali lilikuwa changamoto kubwa. Hii imeongeza uwazi na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maji.




Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akizindua rasmi Awamu ya Tatu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliyoanza Julai 2022 hadi Juni 2026.

Aweso pia amekuwa mstari wa mbele katika kusimamia miradi mikubwa ya kimkakati kama Mradi wa Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Simiyu (SCRP), unaogharimu zaidi ya Euro milioni 171.

Mradi huu unaotekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania, Green Climate Fund (GCF), na Serikali ya Ujerumani kupitia KfW, unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa wakazi wa mkoa wa Simiyu.

Mradi huu ni mfano wa mafanikio ya ushirikiano wa kimataifa katika kutatua changamoto za ndani.

Chini ya uongozi wake, taasisi zinazoendeleza mradi huo, zimeweza kuboresha mifumo yao ya kiutawala na kifedha, kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa kama mita za maji za kielektroniki, na kuboresha huduma kwa wateja.

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

KFW


GREEN CLIMATE FUND

Pamoja na miradi hiyo, Waziri Aweso ameweka msisitizo mkubwa katika kuimarisha taasisi na mamlaka za maji nchini.




**“ Chuo cha Maji kitumike kutatua changamoto za maji nchini ”**

Kipengele kingine muhimu ni mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji (NAWAPO 2002), ambayo imeboreshwa. Sera hii imejumuisha masuala mapya kama uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, ushiriki wa sekta binafsi, na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za maji.




Hii inaonesha namna ambavyo Aweso anazingatia mabadiliko ya wakati na kuhakikisha Sekta ya Maji inakwenda sambamba na maendeleo ya dunia.

Sifa kubwa ya Aweso, yeye si kiongozi wa kukaa ofisini pekee. Ni mtu wa kufika katika maeneo ya miradi, kukagua maendeleo ya ujenzi wa miradi ya maji, upatikanaji wa huduma ya maji na kuzungumza na wananchi uso kwa uso.

Akiwa kwenye maeneo hayo, mara nyingi husikika akisema: "Hatutakuwa kikwazo kwa wananchi wa Tanzania kupata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza".

Kauli hii imekuwa kama wimbo katika Sekta ya Maji, ikisisitiza umuhimu wa kutenda kwa moyo, haraka na kwa ufanisi.

Chini ya uongozi wa Aweso, Sekta ya Maji nchini Tanzania imeimarika kwa kiasi kikubwa. Takwimu zinaonesha ongezeko la wananchi wanaopata huduma ya majisafi na salama, huku maeneo mengi ya vijijini na mijini yakiunganishwa na huduma hizo.



**“Hali ya maisha imebadilika sana baada ya miradi ya maji kufika karibu yetu”**

**Mama Hadija Rajabu**
**Mkazi wa Simiyu**



**“ Chini ya Waziri Aweso, Sekta ya Maji imepata msukumo mpya. Sasa tunazungumza kuhusu matokeo, si tena kupanga mikakati ya karatasi bila utekelezaji ”**

**Mhandisi Mwajuma Waziri**
**Katibu Mkuu Wizara ya Maji**

Aweso pia amekuwa akihimiza kuwajengea uwezo wataalamu wa Sekta ya Maji. Mafunzo ya mara kwa mara yamekuwa yakitolewa kwa wahandisi, mafundi, na maafisa huduma kwa wateja ili kuhakikisha wanakuwa na ujuzi wa kisasa. Hii ni sehemu ya mkakati wake wa kuhakikisha sekta ya maji inakuwa na watu wenye uwezo wa kusimamia miradi kwa weledi.

Licha ya mafanikio haya yote, Waziri Aweso amekiri mara kadhaa kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya. Anasisitiza kuwa Serikali itaendelea kuongeza nguvu katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na huduma za maji, hasa vijijini na katika maeneo yenye changamoto za kijiografia.

Kutoka kuwa Mwalimu wa Kemia hadi kuwa Waziri wa Maji, safari ya Jumaa Hamidu Aweso ni mfano wa uongozi thabiti, maono, na kujituma vinavyoweza kubadili maisha ya wananchi. Ni simulizi ya kijana kutoka Pangani aliyeamua kutumikia taifa kwa moyo wa dhati, akihakikisha kuwa kila Mtanzania anapata huduma ya maji safi na salama.

Katika historia ya Sekta ya Maji Tanzania, jina la Jumaa Aweso sasa linatajwa miongoni mwa viongozi walioweka alama ya kudumu, wakihakikisha kuwa Tanzania inafikia lengo la upatikanaji wa huduma ya maji kwa wote ifikapo mwaka 2030.

# Historia ya Uongozi katika Wizara ya Maji (Mawaziri)

Katika kipindi chote cha historia ya Wizara ya Maji, mawaziri mbalimbali wameongoza, kila mmoja akiacha alama yake. Baadhi ya Mawaziri waliowahi kuiongoza Wizara hii ni pamoja na:



**Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete**
**1990 - 1995**



**Mhe. Jackson Makweta**
**1995 - 1995**



**Mhe. Dkt. Pius Ng'wandu**
**1996 - 1999**



**Mhe. Mussa Nkhangaa**
**1999 - 2000**



**Mhe. Edward Lowassa**
**2001 - 2005**



**Mhe. Steven Wassira**
**2005 - 2006**

# Historia ya Uongozi katika Wizara ya Maji (Mawaziri)



Mhe. Dkt. Shukuru Kawambwa
2007 - 2008



Mhe. Prof. Mark Mwandosya
2008 - 2012



Mhe. Prof. Jumanne Maghembe
2012 - 2015



Mhe. Eng. Gerson Lwenge
2015 - 2017



Mhe. Eng. Isaac Kamwelwe
2017 - 2018



Mhe. Prof. Makame Mbarawa
2018 - 2020



**Mhe. Jumaa Aweso (Mb)**
**2020 - 2025**




# Miaka Nane ya Mafanikio Makubwa Sekta ya Maji

**Uongozi wa kisera, ambapo Tanzania inaongoza utekelezaji wa Programu ya Malipo kwa Matokeo (PforR) duniani, na imeanzisha Hati Fungani ya Kijani yenye thamani ya Shilingi Bilioni 54.72.**




# Kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 Toleo la Mwaka 2025



# Kukamilika kwa Miradi 2,331 ya Maji

# Ikiwemo Miradi Mikubwa ya Maji

**Ujenzi wa jumla ya miradi 2,331 ya maji, ikiongeza huduma vijijini kutoka asilimia 70.1 (2020) hadi asilimia 83 (Desemba 2024), na mijini kutoka asilimia 84 hadi asilimia 91.6.**

# Mradi wa Same - Mwanga - Korogwe






Mradi
wa Maji
Kyaka-Bunazi
Unahudumia
wakazi 35,000 wa
kata za Kyaka na
Kasambya



**Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu akizindua mradi wa maji Butimba pamoja na mtambo wa kutibu maji katika eneo hilo.**



**Muonekano wa chanzo cha maji Butimba pamoja na Mtambo wa kutibu maji katika eneo la Butimba.**

# Kuanza Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati





Bwawa la Kidunda
(Tshs. 329.46 Bilioni)

## Miradi ya Maji ya Miji 28 (Trilioni 1.6)



## Mradi wa Maji kwenda Haydom (Bilioni 41)



## Mradi wa Bwawa la Farkwa (Bilioni 312.08)



## Mradi wa Maji kutoka Kahama kwenda Ushetu (Bilioni 42)





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi Simiyu (Bilioni 440)



**Mradi wa Maji Ukirigulu, Koromije, hadi Sumve (Bilioni 32)**



Kuongezeka kwa bajeti ya Wizara kutoka Shilingi Bilioni 680 (2021/22) hadi Shilingi Trilioni 1 (2025/26).




**Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango akizindua uuzaji wa hati fungani ya kijani kwa ajili ya mradi wa maji Tanga.**




**Waziri Aweso akiongea katika hafla ya hati fungani ya kijani ya Tanga UWASA kusajiliwa rasmi kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)**

Kuimarika kwa ushirikiano na Jumuiya za Kimataifa, ambapo fedha nyingi zimepatikana kutoka Benki ya Dunia, na nchi za India, Korea Kusini, Ufaransa, Hungary pamoja na Mifuko ya Mabadiliko ya Tabianchi.








KUBORESHWA
KWA MAZINGIRA
YA KAZI













# Kuboreshwa kwa mazingira ya kazi

## Kuanzishwa kwa mchakato wa ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji.




Rais Dkt. Samia amemuagiza Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) kuanzisha Gridi ya Maji ya Taifa





# Mambo ya Kipekee Kuhusu Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb)

Umahiri mkubwa katika kujibu hoja na maswali Bungeni, akiwa Waziri mwenye weledi akizijua kero za wananchi (anayelala na mgonjwa ndiyo anayejua mihemo ya mgonjwa), na amekuwa akijibu hoja na maswali ya Bunge kwa ufasaha, maarifa na ushawishi mkubwa.





## Mambo ya Kipekee Kuhusu Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb)

Ametembelea majimbo yote ya Tanzania Bara, hakuna eneo ambalo halijaguswa na Waziri Aweso kwa kutembelea miradi kila kona ya nchi kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wake.





**Kama Waziri, amekua mstari wa mbele katika kampeni ya "Kumtua Mama Ndoo Kichwani"**





# “Amefia Site”



Ni Waziri ambaye muda wake mwingi umekuwa kwenye maeneo ya miradi kuliko ofisini akitoa maagizo kwa wakandarasi kufanya kazi hadi usiku kwa ajili ya wananchi.





**Ni Waziri mdogo zaidi kiumri katika historia ya Sekta ya Maji, kuteuliwa kwake akiwa na umri mdogo kumethibitisha kuwa uongozi ni suala la uwezo, dhamira na uchapakazi wala si umri.**





Kwa ufupi Aweso “ameupiga mwingi sana”

# Hitimisho

Kwa miaka mitano mfululizo akiwa waziri kamili wa maji, Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso (Mb) ameiongoza Sekta ya Maji kwa ufanisi wa hali ya juu, na kwa usimamizi wa karibu wa miradi na matumizi ya fedha za umma. Sekta ya Maji leo ni mfano wa uwajibikaji, usimamizi na ubunifu. Pamoja na mafanikio hayo yapo maeneo yanayoibeba sekta na yanahitaji kuimarishwa ili kufikia malengo zaidi:-



01

Kuongeza bajeti ya Mfuko wa Taifa wa Maji kufikia Shilingi bilioni 400 kwa mwaka ili uchangie hadi asilimia 50 ya bajeti ya Wizara kutoka vyanzo vya ndani.

02

Kuendeleza ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, na mito mikubwa kama Rufiji na Ruvuma.

03

Kuifanya Sekta ya Maji kuwa kichocheo cha uchumi wa viwanda, kilimo, afya, elimu na usalama wa chakula na taifa (maji ni uchumi).



**“Ni imani yangu kuwa Tanzania itaendelea kutumia rasilimali maji kama nyenzo kuu ya maendeleo ya watu wake. Maji ni uhai, lakini pia ni usalama. Bila maji hakuna chakula, hakuna afya, hakuna uzalishaji, hakuna usalama, hakuna mustakabali wa taifa”**



**Mhe. Jumaa Aweso (Mb)**
**Naibu Waziri wa Maji**
**2017-2020**
**Waziri wa Maji**
**2020-2025**



Imeandaliwa na:
Wizara ya Maji
Mji wa Serikali, 6 Mtaa wa
Kisima, S.L.P 456, 40473
Dodoma.

www.maji.go.tz

majiDigital wizarayamajitz